# Kurudisha Njia Za Zamani
# (Restoring The Old Paths)

**Na**

**John Kombo**

# Kurudisha Njia Za Zamani (Restoring The Old Paths)

**Na**

**John Kombo**

**May 15, 2014**

# Kurudisha Njia Za Zamani

"*BWANA asema hivi, simameni katika njia kuu mkaone mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema hatutaki kwenda katika njia hiyo.*" (Yer. 6:16).

Kauli hiyo hapo juu umekuwa ni usia wa nguvu wa nabii wa Mungu katika historia yote. Agano la Kale limejaa na shauri dhidi ya shauri ya watu wa Mungu wakiacha njia za Mungu na kuinuka kwa manabii wakihubiri toba na urejesho. Wakati wa Agano la Kale Mungu aliwatuma manabii wake na ujumbe kama ulio katika Yeremia 6:16. Lakini walikataa kusikia na kusema, "hatutaki kwenda katika njia hiyo."

Roho Mtakatifu aliwavuvia watu arobaini kuandika Bibilia (2 Tim. 3:16). Leo watu wanasoma kitabu kilichoandikwa na Mungu, lakini bado wamesema, "tutasoma kitabu chako lakini hatutasikia wala kufanya kile unachosema (Luka 6:46).

Dunia ya leo haiku tofauti sana, nasi pia tuna paswa kufundisha toba na urejesho, tunatakiwa kurudi katika njia ya "zamani". Wakati kanisa la Bwana wetu lilipoanzishwa, (30 AD) uliza Wakristo wa karne ya kwanza waliabuduje; kwa mfano: waliimbaje? Walishirikije meza ya Bwana? Walihibiri nini? Walitoa vipi na ni katika siku gani? Kanisa lilikuwa na mpangilio gani? Tunaweza tu kupata taarifa zote kwa kusoma na kujifunza Agano lao Jipya toka wakati ambapo kanisa lilipoanzishwa (Mdo. 2:14-47). Alafu endelea kusoma nyaraka za Mtume Paulo kwa makusanyiko tofauti Palestina na kuendelea.

Mimbari zetu na madarasa za Biblia zinapaswa kupiga kengele kwa neno, "*Bwana asema hivi*" au "Biblia inasema" kwa wakati huu ambao tuna maneno yaliyoandikwa. Tunaweza kuwaongoa wanaume kwa wanawake kwa Mungu na kuwa marafiki wa Biblia pekee tutaacha kucheza na kuingia katika mambo ya msingi – hiyo ni kujifunza Biblia, kutoka katika kitabu cha kwanza Mwanzo, hadi katika kitabu cha mwisho cha Ufunuo wa Yohana tukiwapa wale tuliojaliwa kuwafundisha. Hii inapaswa kuchukuliwa kwa maantiki kama inavyohusu mambo ya umilele.

Yuda anatuhimiza kwa kusema kwa wale aliowaandikia "*Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*" (Yuda 3).

Ndugu zangu wapendwa, tuna wajibu kwa Mungu "*kuishindania imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*" Tunawajibu na majukumu kwa mwanadamu kutafuta "njia ya zamani"; tunapoongea na "*tuongee yale yaliyo maagizo ya Mungu.*"

Mungu awabariki na neno la Mungu likae kwa wingi ndani yenu.

John Kombo Nandwa

Kanisa la Kristo Barut

Nakuru, Kenya